

**MKATABA WA KUUZIANA SHAMBA.**

MKATABA huu umefanyika hapa Mwanza leo Tarehe 18 Mwezi 05 2024.

**BAINA YA**

**JOHN PATRICK MASOLOLO** wa S. L. P 1013 MISUNGWI, MWANZA TANZANIA (ambae katika Mkataba huu ataitwa "MUUZAJI") neno litakalowahusu warithi wake, mawakala, na mtu mwingine yeyote atakayedai kwa niaba yake kwa upande mmoja.

**NA**

**MENGI INTERNATIONAL DRILLING LIMITED** wa S. L. P 2837 MWANZA TANZANIA (ambae katika Mkataba huu ataitwa "MNUNUZI") neno litakalowahusu warithi wake, wakala, na mtu mwingine yeyote atakayedai kwa niaba yao, kwa upande mwingine.

**KWA KUWA**

- A. MUUZAJI ni mmiliki halali wa shamba ambalo halijapimwa lililopo kitongoji cha KIGONGO, BUSISI wilaya ya MISUNGWI-MWANZA lenye ukubwa wa MITA ZA MRABA 4,000 Na yuko tayari kuuza eneo hilo kwa mnunuzi.
- B. Mipaka ya shamba tajwa ni kama ifuatavyo: upande wa kaskazini limepakana na barabara, upande wa mashariki limepakana na NEEMA MASUMBUKO, Magharibi limepakana na barabara kuu, Kusini limepakana na ELIAS MANGUNGU.

**MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO: -**

1. Bei ya mauziano ni **Shilingi za Tanzania Milioni Hamsini Taslim (Tshs.50,000,000/=)**, ambazo zimelipwa kwa awamu moja siku ya kusaini mkataba huu,
2. Kwamba, shamba hilo linauzwa bila kipingamizi chochote, rehani, tahadhari au madai ya aina yoyote ile. Endapo itagundulika baadaye kuwa muuzaji hakuwa mmiliki halali atarejesha kwa Mnunuzi pesa za mauziano na gharama zote atakazo kuwa ameingia kuhusiana na mauziano hayo.
3. Kwamba, gharama za kushughulikia upimaji na upatikanaji wa Hati miliki zitakuwa ni juu ya Mnunuzi.
4. Kwamba, Wahusika wameingia mkataba huu wakiwa na akili timamu bila kulazimishwa au kuahidiwa chochote na mtu yoyote kwa manufaa yoyote.
5. Kwamba, pande zote zimekubaliana kuwa Mkataba huu utalindwa na sheria ya Mkataba Sura Na. 345 iliyorejewa mwaka 2019 na sheria nyinginezo zinazoendana hapa Nchini.

**KWA KUSHUHUDIA HAYA** wahusika wote wameweka saini zao katika Mkataba huu katika tarehe na kwa namna kama inavyoonyesha hapa chini: -

**UMESAINIWA na KUKUBALIWA Hapa Mwanza**  
na **JOHN PATRICK MASOLOLO** ambae  
namfahamu binafsi /nimetambulishwa na  
HAMIS WINGA  
leo tarehe 18 mwezi 05 2024.

J. Masololo  
MUUZAJI

**MBELE YANGU:**

JINA: \_\_\_\_\_  
SAHIHI: \_\_\_\_\_  
ANUANI: \_\_\_\_\_  
CHEO: **WAKILI**

**UMESAINIWA NA KUKUBALIWA hapa Mwanza**  
**MENGI MOSHI LUMAMBO/MKURUGENZI WA**  
**MENGI INTERNATIONAL DRILLING LIMITED**  
ambae namfahamu binafsi /nimetambulishwa  
na ANDREW WILUUM  
leo tarehe 18 mwezi 05 2024.

Andrew Wiluum  
MNUNUZI

**MBELE YANGU:**

JINA: PRINCE CAROL RAIJIB  
SAHIHI: [Signature]  
ANUANI: 24393  
CHEO: **WAKILI**



**UMEANDALIWA NA:**  
PANDE MBILI ZA MKATABA